TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI **1/11/2017**

- **Maonyesho ya mitindo ya "Swahili Fashion Week" kusherekea miaka 10 toka ilipo anzishwa.**
- **Zaidi ya wabunifu 50 kusherekea miaka maadhimisho ya miaka 10 ya Swahili Fashion Week Disemba 1, 2, & 3.**
- **Swahili Fashion Week kufanyika tarehe 1, 2, & 3 Disemba mwaka huu**.

Msimu wa mitindo umefika, maandalizi ni ya kupendeza na yamejaa purukushani sababu ya kusherekea miaka ya mafanikio na ukuu wa maonyesho haya ya Swahili Fashion Week toka yalipo anzishwa. Hakika ni hatua kubwa! Mwezi wa disemba mwaka huu, sekta ya mitindo Tanzania watakuwa na furaha ya kutimiza miaka kumi ya jukwaa kubwa la mavazi kwa Afrika Mashariki na Afrika ya Kati lijulikanalo kama "**SWAHILI FASHION WEEK & AWARDS**", maonesho haya yatafanyika tarehe 1, 2, na 3 katika ukumbi wa Makumbusho ya Taifa Posta, jijini Dar es Salaam, Tanzania.

Katika kutekeleza mafanikio ya nguvu ya misimu nane iliyopita, jukwaa la Swahili Fashion Week linachukuliwa si vinginevyo Zaidi ya kuwa jukwaa la mitindo linaloongoza Afrika katika upande wa kukuza vipaji, uvumbuzi wa mitindo na utunzaji wa tamaduni za Kiswahili. Mwanzilishi wa maonyesho haya ya kifahari, kwa moyo wa dhati anasema, " Tunasherekea mafanikio ya sekta yetu ya mitindo, tukilenga kukuza maeneo yote na kuendeleza maonyesho yanayofata ya Swahili Fashion Week, Pamoja na wadhamini wetu na wabunifu tunachukua mafunzo mazuri ya kimataifa na kuchanganya na ya hapa nchini ili kupata vitu vizuri vitakavyo wawezesha wabunifu wetu wa hapa nchini, lazima tuzingatie biashara nzuri za wabunifu na tuweze kupeleka nembo zao katika hatua za kimataifa.

Mustafa anaongeza kuwa,"lengo letu kubwa si tu kutangaza na kusherekea maonesho haya ya Swahili Fashion Week, bali kusaidi kutekeleza hujudi za Rais Wetu wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John P Magufuli, katika sera ya kuelekea uchumi wa viwanda kupitia bidhaa za nguo "**zilizotengenezwa Tanzania** ", kama alivyosema katika hotuba yake ya utambulisho mwaka 2015. Hivyo basi, tunawaomba vyombo vya habari na wadau wengine kusherekea nasi kwa kuwaunga mkono wabunifu wetu wa mitindo na kushuhudia mitindo ya kipekee katika maonyesho haya. Kama methali hii ya Afrika inavyosema "kama unataka kwenda haraka nenda mwenyewe, kama unataka kwenda mbali nenda pamoja"

Hatua kubwa ya miaka kumi ya Swahili fashion week, itawaacha watu midomo wazi na kuendelea kuwa kivutio katika maonyesho yote ya mitindo nchini Afrika, pamoja na wabunifu wa ndani na kimataifa wakipata hisia za dhata kutoka kwa vyombo vya habari vya nchini na nje ya nchi toka maonesho haya yalipoanzishwa mwaka 2008. Swahili fashion week limekuwa jukwaa la kwanza lenye ubunifu kwa wabunifu wa mitindo kutoka Afrika Mashariki na kwengineko ambao uonyesha mavazi yao kwa ulimwengu.

"Tukisherekea maadhimisho ya miaka 10, tunakazania katika watu wanaoboresha sekta ya mitindo ya Afrika Mashariki, pamoja na bidhaa zenye mvuto wa kimataifa, ni fahari kwa jukwaa hili kuwa sehemu ya ukuaji wa mitindo kwa Afrika Mashariki, huku tukishuhudia ukuaji mzuri wa wabunifu na wanamitindo. Tofauti na maonyesho ya miaka iliyopita, onyesho la kumi la Swahili Fashion Week litakuwa na mabadiliko makubwa ambayo yanajumuisha utoaji wa tuzo kwa siku zote tatu za maonyesho." Alisema Meneja mradi wa Swahili Fashion Week, Glory Urassa

Mwaka huu maonyesho ya Swahili Fashion Week na Tuzo yatafanyika jioni kuanzia tarehe 1- 3 Disemba katika ukumbi wa Makumbusho ya Taifa, yakiwa na wabunifu Zaidi ya 50 kutoka nchini na nje ya nchi. Nyakati za jioni kuanzia saa kumi na mbili hadi saa nne usiku kutakuwa na bazaar na muziki wa band, wajasiliamali mbalimbali wataonesha bidhaa zao za kazi za mikono, Sanaa na vito, sambamba na sehemu ya mapaumziko kwa watu maalum itakuwepo kwa wale wanaotaka kutumia jioni yao wakiwa pamoja na watu maarufu, watu wa mitindo na vyombo vya habari huku wakiburudika na maonyesho makubwa ya mitindo Tanzania.

Maonyesho ya Swahili Fashion Week yameandaliwa na 361 Degrees Africa na kudhaminiwa na Azam Tv, Italian Trade Agency, Golden Tulip Hotel, Fasjet, BASATA, Asila's Makeup, Fabcars, Huayuan Security, Nexia SJ, GreenTelecom, Epidor, Michuzi Blog ,Eventlite, African Stars na Majira.

KUHUSU SWAHILI FASHION WEEK

Swahili fashion week ni onyesho kubwa la mitindo na mavazi afrika mashariki na kati linaliofanyika kila mwaka, ni jukwakaa kubwa linalowapatia nafasi wabunifu wa mavazi na vito kutoka nchi za afrika masharika na zinginezo kuonyesha vipaji vyao, kutengeneza soko la ubunifu na kupata na kukuza mtandao wa wateja katika tasnia ya mitindo.

onyesho hili lina nia ya kusisitiza jamii kuwa mitindo ni pato linalozalisha tasnia ya ubunifu, wakati huo huo ikikuza dhana ya "bidhaa za afrika ". Swahili fashion week ni jukwaa la mitindo lilianzishwa mwaka 2008 na Mustafa Hassanali mbunifu kubwa na mkongwo afrika kutoka Tanzania.

Swahili Fashion Week ni jukwaa la mitindo lilianzishwa mwaka 2008 na mbunifu mkongwe na mashuguhuli kutoka Tanzania, Mustafa Hassanali

Onyesho la mwaka huu litakuwa onyesho la 10 toka lianze kufanyika.

Media Inquiries

Maryam@361africa.com

+255785862323